ewura
Energy and Water Utilities Regulatory Authority
ISO 9001:2008 Certified

**Ghorofa ya Saba, LAPF Pensions Fund Tower; Mkabala na Kijiji cah Makumbusho, Kijitonyama; S.L.P 72175, DAR ES SALAAM; Simu: +255-22-2923513/8; Nukushi:+255-22-2923519**
Barua Pepe: info@ewura.go.tz Tovuti: http.//www.ewura.go.tz

# TANGAZO KWA UMMA

## MWITO WA MAONI YA WADAU KUHUSU MAOMBI YA MAREKEBISHO YA BEI ZA MAJI KUTOKA MAMLAKA YA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA MAKAMBAKO ("Makambako WSSA") KWA MWAKA 2016/17 – 2018/19

**Maombi ya mabadiliko ya Bei Na. TR-W-16-021**

Mnamo tarehe 3 Machi 2017 Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), ilipokea maombi yaliyokamilika kutoka Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Makambako (Makambako WSSA) ya kutaka kuongeza bei ya huduma zake za majisafi kwa mwaka 2017/18 hadi 2019/20. Jedwali namba 1 hadi 5 hapa chini yanaonesha mchanganuo wa bei za sasa na zinazopendekezwa.

**Jedwali Na 1: Bei za Sasa na Zinazopendekezwa kwa Wateja Wenye Dira (Shilingi kwa Uniti moja ya ujazo)**

| Kundi la Wateja | Kiwango cha Matumizi kwa uniti | Bei za Sasa | Bei Zinazopendekezwa | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2016/17 | Mabadiliko kwa asilimia | 2017/18 | Mabadiliko kwa asilimia | 2018/19 | Mabadiliko kwa asilimia | 2019/20 |
| Majumbani | 0-10 | 3,000 | 39% | 549 | 9% | 598 | 4% | 622 |
| | >10 | 395 | | | | | | |
| Biashara | 0- 20 | 8,000 | 39% | 709 | 9% | 773 | 4% | 804 |
| | >10 | 510 | | | | | | |
| Taasisi | 0-25 | 10,000 | 39% | 695 | 9% | 758 | 4% | 788 |
| | >25 | 500 | | | | | | |
| Magati | >0 | 500 | 39% | 695 | 0% | 695 | 0% | 695 |
| Ujenzi | >0 | 1,000 | 39% | 1,390 | 9% | 1,515 | 4% | 1,576 |
| Viwanda | 0-25 | 15,000 | 39% | 994 | 9% | 1,083 | 4% | 1,126 |
| | >25 | 715 | | | | | | |

**Jedwali Na. 2: Bei za Sasa na Zilizopendekezwa kwa Wateja wasio na Dira (Shilingi/Mwezi)**

| Kundi la Wateja | Bei za Sasa | Bei Zinazopendekezwa | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2016/17 | Mabadiliko kwa asilimia | 2017/18 | Mabadiliko kwa asilimia | 2018/19 | Mabadiliko kwa asilimia | 2019/20 |
| Majumbani | 4,500 | 100% | 9,000 | 50% | 13,500 | 25% | 16,875 |

**Jedwali Na.3: Tozo ya Huduma ya Sasa na Inayopendekezwa (Shillingi/Mwezi)**

| Kundi la Wateja | Tozo za sasa | | Tozo Zinazopendekezwa | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2016/17 | Mabadiliko kwa asilimia | 2017/18 | Mabadiliko kwa asilimia | 2018/19 | Mabadiliko kwa asilimia | 2019/20 |
| Majumbani | 0 | NA | 2,000 | 50% | 3,000 | 25% | 3,750 |
| Biashara | 0 | NA | 3,000 | 50% | 4,500 | 25% | 5,625 |
| Taasisi | 0 | NA | 3,000 | 50% | 4,500 | 25% | 5,625 |
| Magati | 0 | NA | 2,000 | 50% | 3,000 | 25% | 3,750 |
| Ujenzi | 0 | NA | 3,500 | 50% | 5,250 | 25% | 6,563 |
| Viwanda | 0 | NA | 3,500 | 50% | 5,250 | 25% | 6,563 |

**Jedwali Na.4: Ada za Sasa na Zinazopendekezwa za Kurejeshewa Huduma Baada ya Kukatiwa huduma (Shilingi/Kurejeshewa huduma)**

| Kundi la Wateja | Ada za Sasa | Ada zinazopendekezwa | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2016/17 | Mabadiliko kwa asilimia | 2017/18 | Mabadiliko kwa asilimia | 2018/19 | Mabadiliko kwa asilimia | 2019/20 |
| Majumbani | 10,500 | 100% | 21,000 | 0% | 21,000 | 30% | 27,300 |
| Biashara | 16,000 | 100% | 32,000 | 0% | 32,000 | 30% | 41,600 |
| Taasisi | 16,000 | 100% | 32,000 | 0% | 32,000 | 30% | 41,600 |
| Ujenzi | 15,000 | 100% | 30,000 | 0% | 30,000 | 30% | 39,000 |
| Viwanda | 16,500 | 100% | 33,000 | 0% | 33,000 | 30% | 42,900 |

**Jedwali Na.5: Ada ya Maunganisho ya Huduma ya Maji ya Sasa na Inayopendekezwa (Shilingi kwa Maunganisho)**

| Kundi la Wateja | Ada za Sasa | | Ada zinazopendekezwa | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2016/17 | Mabadiliko kwa asilimia | 2016/17 | Mabadiliko kwa asilimia | 2016/17 | Mabadiliko kwa asilimia | 2016/17 |
| Majumbani | 32,000 | 56% | 50,000 | 25% | 62,500 | 20% | 75,000 |
| Biashara | 33,000 | 97% | 65,000 | 30% | 84,500 | 25% | 105,625 |
| Taasisi | 33,000 | 97% | 65,000 | 30% | 84,500 | 25% | 105,625 |
| Ujenzi | 33,000 | 112% | 70,000 | 30% | 91,000 | 25% | 113,750 |
| Viwanda | 33,000 | 142% | 80,000 | 30% | 104,000 | 25% | 130,000 |

MAKUWASA imeeleza kuwa, bei zinazopendekezwa zitaisaidia kupata fedha ya kutosha kugharimia gharama za uendeshaji na matengenezo ambazo zimeongezeka kama vile gharama za umeme na madawa ya kutibu maji. Pia, MAKUWASA imeeleza kuwa, ongezeko linalopendekezwa litaisaidia kuzingatia Dira na Maono ya MAKUWASA na malengo iliyojiwekea kwa mwaka 2017/18 – 2019/20 ili kuhakikisha kuwa idadi ya watu wenye maji safi na salama inafikia asilimia 70 ifikapo mwaka 2019.

Kwa mujibu wa kifungu Na. 19 (2) (b) cha Sheria Na. 414, kutakuwa na Mkutano wa Taftishi siku ya **Alhamisi, tarehe 4 Mei 2017 katika Ukumbi wa Green City uliopo mji wa Makambako** kuanzia saa **4:00 asubuhi** kwa ajili ya kupata maoni ya wadau ikiwa ni pamoja na Baraza la Ushauri la Serikali na Baraza la Ushauri la watumia Huduma zinazodhibitiwa na EWURA na wananchi wote kwa ujumla kuhusu uhalali wa bei zinazopendekezwa.

Wadau wanaopenda kutoa maoni kwa maandishi wanaombwa kufanya hivyo kwa kutuma maoni yao kwa Mkurugenzi Mkuu wa EWURA kwa anuani iliyoonesha hapo juu **ifikapo 8 Mei 2017**. Maelezo zaidi yanaweza kupatikana katika ofisi ya EWURA, **GHOROFA YA SABA, LAPF PENSIONS FUND TOWER; MKABALA NA KIJIJI CHA MAKUMBUSHO, KIJITONYAMA, DAR ES SALAAM** au **ofisi za Mamlaka ya Maji Makambako.**

**Imetolewa na:**
**Mkurugenzi Mkuu**
**Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA)**

**11 Aprili 2017**